Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

# ELIMU Bulletin

JARIDA LA MTANDAONI: *Toleo Na.43* - **2025**

wizara_elimuTanzania wizara_elimuTz www.facebook/moestvt.com www.wyestu.blogspot.com www.moe.go.tz ELIMUTZ

*Tunaboresha Elimu Yetu*






# Elimu ya Watu Wazima nyenzo muhimu kujikomboa kiuchumi - Mhe. Majaliwa

**- KAZI IENDELEE -**

# TAHARIRI

## Miaka 50 ya TEWW - Safari ya Maarifa bila Kikomo

Mnamo Agosti 25, 2025, Tanzania imeadhimisha miaka 50 tangu kuanzishwa kwa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW), taasisi ambayo imekuwa nguzo muhimu katika kuendeleza elimu jumuishi kwa Watanzania wote. Maadhimisho haya yameongozwa na kauli mbiu **"Elimu Bila Ukomo kwa Maendeleo Endelevu"** kauli inayodhihirisha dhamira ya taifa kuhakikisha kila Mtanzania, bila kujali umri, hali ya kijamii au mahali alipo, anapata fursa ya kujifunza na kujiendeleza

Kwa kipindi cha miaka 50, TEWW imekuwa mshirika wa karibu wa Serikali katika kushauri sera, kutekeleza miradi ya kimkakati kama SEQUIP na IPOSA, na kuwafikia makundi yaliyoko nje ya mfumo rasmi wa elimu. Kupitia utekelezaji wa programu hizo Wasichana zaidi ya 13,000 wameweza kurejea shuleni, na vijana 10,000 wamepata stadi za maisha na ujasiriamali kupitia programu hizi.

Akizungumza katika kilele cha maadhimisho hayo, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa, alisisitiza kuwa elimu ya watu wazima siyo tu njia ya kuongeza maarifa na ujuzi, bali ni nyenzo muhimu ya kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Alieleza kuwa mafanikio ya TEWW ni ushahidi wa dhamira ya Serikali ya kuhakikisha hakuna Mtanzania anayebaki nyuma katika safari ya maendeleo

Aidha, tumeshuhudia Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imeendelea kuonesha uongozi thabiti kwa kuweka sera madhubuti, kusimamia kwa makini utekelezaji wa programu, na kuwezesha rasilimali zinazohitajika.

Matokeo yake ni TEWW kuwa nguzo imara ya kuwainua Watanzania waliokosa fursa za awali za elimu, na hivyo kuchochea ushiriki wao kupitia mfumo wa sasa wa Elimu bila Ukomo.

Mafanikio haya si tu kielelezo cha uwekezaji wa Serikali katika maarifa, bali pia ni mwanga wa matumaini kwa vizazi vijavyo. Ni ushuhuda kuwa elimu haina kikomo, na kwamba kila hatua ya kujifunza ni mchango katika ujenzi wa taifa lenye usawa, ustawi na maendeleo endelevu.

**Elimu na Ujuzi Mpango Mzima.**






**BODI YA UHARIRI**

**Sylvia Lupembe**
*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini*

**Wachangiaji:**
Oliva Kato
Elizabeth Pancras
Veronica Chitunda
Nazareth Mwakabuta

**Mawasiliano:**
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Afya - Dodoma
S.L.P. 10, 40479 DODOMA.
Simu: +255 26 296 3533

**Jarida hili linatolewa na**
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Elimu ya Watu Wazima ni Ukombozi >



# Elimu ya Watu Wazima nyenzo muhimu kujikomboa kiuchumi - Mhe. Majaliwa

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, amesema Elimu ya Watu Wazima ni nyenzo muhimu ya kuwawezesha Watanzania kujikomboa kiuchumi na kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya taifa, hivyo ameitaka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuendelea kupanua wigo wa utolewaji wa elimu hiyo.

Akizungumza katika kilele cha Kongamano la Maadhimisho ya Miaka 50 ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kilichofanyika Jijini Dar es Salaam, Agosti 25, 2025, Mhe. Majaliwa amesisitiza umuhimu wa elimu hiyo kuwa jumuishi, inayozingatia mahitaji halisi ya jamii. Aidha, amehimiza kuhakikisha elimu hiyo inawafikia wananchi wote bila kujali hali zao za kiuchumi, umri, au mahali wanapoishi.

Waziri Mkuu ameitaka Taasisi hiyo kuongeza tafiti na ubunifu katika utoaji wa elimu nje ya mfumo rasmi, ili kukabiliana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia. Aidha, amehimiza ushirikiano wa karibu kati ya Wizara na wadau wa elimu katika uwekezaji wa miundombinu, ili kuhakikisha elimu inayotolewa katika vituo vya elimu bila ukomo inakuwa bora na inakidhi mahitaji ya walengwa



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema moja ya mafanikio makubwa ya taasisi hiyo yametokana ni kutekeleza agizo la Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, linalohimiza wanafunzi walioacha shule kurejea masomoni.

Kupitia mpango huo, zaidi ya wanafunzi elfu 13 wamerudi shuleni na kupata elimu nje ya mfumo rasmi. Elimu hiyo imewasaidia kubadilisha maisha yao kwa njia chanya na kuimarisha nafasi yao katika jamii.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo amesema kuwa Kongamano hilo limewakutanisha wadau mbalimbali kujadili kwa kina namna ya kuimarisha upatikananji wa elimu jumuishi kwa makundi yote na kutathimini mafanikio na changamoto ili kuboresha sera na mikakati ya utoaji wa elimu.

Mkuu wa Taasisi hiyo, Prof. Philipo Sanga, amesema kuwa Taasisi hiyo imejipanga kuimarisha utoaji wa huduma kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), ili kuwafikia wananchi wengi zaidi na itaendelea kushirikiana na wadau wadau wa elimu, na kuendelea kutoa elimu kwa makundi mbalimbali ikiwemo maafisa usafirishaji na wageni kutoka nje wanaokuja kujifunza.

Fursa za Ufadhili >

# Serikali inajenga miundombinu ya elimu na kuongeza fursa za ufadhili Elimu ya Juu - Prof. Mkenda







Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda, Agosti 23, 2025 ameweka jiwe la msingi Mradi wa Ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Tukuta iliyopo Kata ya Terat, Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara. Mradi huu unaotekelezwa na ECLAT Development Foundation Tanzania chini ya ufadhili wa Shirika la Upendo la Ujerumani, unagharimu zaidi ya Shilingi Bilioni 4.6.

Waziri Mkenda amelishukuru Shirika hilo, kuwezesha ujenzi wa jumla ya shule 55 nchini, amesisitiza kuwa ushirikiano bado unahitajika katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali ili kuwezesha utekelezaji wa Sera ya Elimu, akikumbusha kuwa ifikapo mwaka 2027, kila mtoto atatakiwa kusoma hadi kufikia kidato cha Nne.

Mkurugenzi wa Shirika la Upendo Foundation Dkt. Fred Heimbach ameipongeza Serikali kwa kufanya uboreshaji na ujenzi wa miundombinu ya elimu, ameitaka jamii kutumia vema fursa hiyo kuhakikisha Watoto wote wanapata elimu bora

Naye, Mwenyekiti wa Kijiji cha Terrat Bw. Kone Medukenya amesema wanajivunia ujenzi wa shule hiyo inayojumuisha vyumba vya madarasa 12, maabara za sayansi 4, mabweni 6, majengo sita ya vyoo, nyumba za walimu 16, jengo la utawala, chumba cha kompyuta na seva, kisima cha maji na miundombinu mingine.

Katika ziara yake mkoani humo, Waziri Mkenda ametembelea Shule ya Sekondari Emboreet iliyopo Kata ya Emboreet, ambapo amewahamasisha wanafunzi kusoma kwa bidii na kutumia fursa mbalimbali za ufadhili wa masomo elimu ya juu ikiwemo Samia Skolashipu kwa fani za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, Elimu Tiba na Hisabati.

Pia amesema mwaka huu Serikali imetangaza ufadhili wa masomo katika ngazi ya Shahada ya kwanza na Shahada ya umahiri kupitia program ya **Samia Scholarship Extended AI/DS** kwa wanufaika wa fani za Data Science, Artificial Intelligence, Cybersecurity, Machine Learning na Allied Science, watakaosoma katika Vyuo Vikuu bora duniani.

Mkuu wa Shule hiyo Aziza Msengese amesema Shule hiyo ya Serikali ilijengwa kwa ufadhili wa ECLAT Development Foundation kwa kushirikiana na Shirika la Upendo la Ujerumani na inajivunia mafanikio mbalimbali ikiwemo ongezeko la ufaulu kwa wanafunzi.

Samia Scholarship DS/AI+ >




# 50 wapata ufadhili wa Samia Scholaship Extended fani za Akili Unde na Sayansi ya Data

Wahitimu 50 waliofanya vizuri katika masomo ya Sayansi kwenye matokeo ya Kidato cha Sita mwaka 2025 wamechaguliwa kupata ufadhili wa Samia Scholarship Extended, kusomea programu za Akili Unde, Sayansi ya Data na Sayansi zingine Shirikishi katika vyuo vikuu mahiri duniani.

Taarifa hiyo imetolewa Agosti 31, 2025 jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo, ambaye amesema kuwa wahitimu waliochaguliwa walitokana na ufaulu wao bora katika masomo ya PCM, PMC na PGM.

Prof. Nombo amesema kuwa wanafunzi hao watawekwa katika Kambi Maalumu ya Maarifa (Boot camp), ambapo watapatiwa mafunzo ya kujenga misingi katika matumizi ya kompyuta, programu na uchambuzi wa mifumo, pamoja na kusaidiwa kufanya maombi ya udahili katika vyuo vya nje kwa kushirikiana.

Ameeleza kuwa mafunzo hayo yatatolewa na wataalamu wabobezi kutoka ndani na nje ya nchi, wakiwemo kutoka sekta binafsi na diaspora, kwa kipindi cha miezi 10.

Aidha watapata fursa ya kufanya mitihani itakayowawezesha kupata vyeti vya kitaaluma mfano IBM, Certificate-Machine Lerning for for Data Science Projects, Certified Certificate in Cyber Security Standards na AWS Certified Cloud Practitioner vinavyotambulika kimataifa.

Ufadhili huu ni utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, toleo la 2023, inayolenga kutoa elimu inayozingatia ujuzi kulingana na soko la ajira na stadi za karne ya 21 ili kuchangia katika maendeleo ya Taifa na kimataifa.



Shahada za Umahiri >

# Vijana 10 waagwa kwenda Ireland kusoma Shahada za Umahiri





Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Daniel Mushi, amesema kuwa Serikali ya Tanzania inaendelea kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha vijana wanapata fursa za elimu na ujuzi unaoendana na mahitaji ya dunia ya sasa.

Akizungumza tarehe 15 Agosti 2025 katika semina maalum ya kuwaaga Watanzania 10 waliopata ufadhili wa masomo ya Shahada ya Umahiri (Masters) kutoka Serikali ya Ireland kupitia Ubalozi wa Ireland nchini Tanzania, Prof. Mushi amesisitiza umuhimu wa kuandaa nguvu kazi yenye uwezo wa kushindana kimataifa.

''Tunaishi katika dunia inayobadilika kwa kasi kubwa, hivyo hatuwezi kubaki nyuma kama watazamaji; tunapaswa kuandaa nguvu kazi yetu ili iweze kuendana na kasi ya mabadiliko hayo," amesema Prof. Mushi.

Amewahimiza wanufaika hao kutumia kikamilifu fursa waliyoipata kwa kuzingatia ubora wa kitaaluma, na kuhakikisha wanarejea nyumbani wakiwa na maarifa na ujuzi utakaosaidia kuchochea maendeleo ya taifa.

Kwa upande wake, Balozi wa Ireland nchini Tanzania, Mhe. Nicola Brennan, amewapongeza washindi hao kwa kufaulu mchakato wa ushindani mkali, akieleza kuwa waombaji walikuwa wengi lakini Watanzania 10 walijitokeza na kuibuka kidedea.

"Tunajivunia sana nyinyi kwa kupata fursa hii. Hakikisheni safari hii inakuwa na maana kwa kuleta ujuzi na maarifa ambayo yanatarajiwa katika maeneo mnayokwenda kusomea," amesema Bi. Brennan.

Miongoni mwa fani ambazo wanafaika hao watazisomea ni shahada ya umahiri kwenye Data Science and Analytics, Architecture, Urbanism & Climate Action, Work and Organisational Behaviour, Global Health, Public Health, International Development, Data Analytics, Sustainable Finance na Robotics and Intelligent.

Mageuzi ya Elimu >




# Vijana ni muhimili katika mageuzi ya elimu nje ya Mfumo Rasmi



Kamishna wa Elimu, Dkt. Lyabwene Mtahabwa, amesisitiza kuwa vijana ni nguzo ya mageuzi ya elimu. Amesema ni muhimu washirikishwe kikamilifu katika mapitio ya miongozo ili iendane na mahitaji ya kizazi cha sasa na kijacho, na kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014, Toleo la 2023.

Dkt. Mtahabwa ametoa rai hiyo Agosti 21, 2025 jijini Dar es Salaam katika mdahalo maalumu uliowahusisha vijana balehe waliopo nje ya mfumo rasmi wa elimu. Ukilenga kukusanya maoni ya vijana kuhusu aina ya ujuzi wanaohitaji ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi.

"Tunahitaji kuhakikisha kuwa elimu nje ya mfumo rasmi inatoa maarifa, maadili, na ujuzi unaoendana na muktadha wa Tanzania, kikanda na kimataifa" amesema Dkt. Mtahabwa.

Ameongeza kuwa, ushirikiano wa karibu na vijana utasaidia kujenga mfumo wa elimu unaoendana na muktadha wa dunia ya sasa, hususan katika nyanja za teknolojia, ajira, na ubunifu.

Vijana walioshiriki mdahalo huo wameeleza changamoto mbalimbali wanazokumbana nazo, ikiwemo; ukosefu wa fursa za mafunzo ya vitendo, kukosa stadi za maisha na mbinu madhubuti za kujiajiri.

Mwakilishi Kiongozi wa Elimu kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) Bi. Simone Vis, amesema shirika hilo linajivunia kushirikiana na Wizara na wadau wengine katika kuleta mageuzi ya elimu. Ameeleza kuwa miradi bunifu inayotekelezwa inalenga kuwawezesha vijana hasa wasichana kujifunza, kujiamini, na kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya jamii.

Maendeleo ya Elimu >

# Serikali ya Tanzania na Italia kuimarisha Taasisi za Elimu ya Ufundi kupitia mradi wa TELMS II

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Italia, kupitia Mradi wa TELMS II, imeazimia kuendeleza mageuzi makubwa katika sekta ya elimu ya ufundi kwa kuimarisha Taasisi za elimu ya ufundi ili kuchochea maendeleo endelevu nchini.

Katika kikao cha Kamati ya Pamoja kilichofanyika tarehe 5 Agosti 2025, Dkt. Kenneth Hosea, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Elimu ya Juu, akimwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, alieleza kuwa Mradi wa TELMS II unatekelezwa kwa bajeti ya Euro milioni 19.79, sawa na Sh. Bilioni 54. Fedha hizo ni mkopo nafuu kutoka Serikali ya Italia kwa Serikali ya Tanzania kupitia makubaliano rasmi ya ushirikiano wa maendeleo.

Dkt. Hosea alifafanua kuwa mradi huo wa miaka mitano (2025-2030) unalenga kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo kwa kuhimiza matumizi ya teknolojia, kukuza ubunifu na ujasiriamali, pamoja na kuimarisha maendeleo ya nishati endelevu na uhifadhi wa mazingira.

Kwa upande wake, Balozi wa Italia nchini Tanzania, Mhe. Giuseppe Sean Coppola, alisisitiza kuwa Serikali ya Italia inajivunia mahusiano chanya ya kidiplomasia na Tanzania, hasa kupitia miradi ya elimu inayolenga kuwajengea Watanzania ujuzi na maarifa kwa maendeleo ya taifa.

Mratibu wa Mradi huo, Dkt. Fredrick Salukele, ambaye pia ni Mkurugenzi wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, alieleza kuwa wanufaika wakuu wa Mradi wa TELMS II ni Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), Chuo cha Ufundi Arusha (ATC), Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume (KIST).

Kikao hicho pia kilihudhuriwa na Makamu Mkuu wa Chuo cha MUST Prof. Aloys Mvuma, Makamu Mkuu wa Chuo ATC Prof. Musa Chacha, Mkuu wa Taasisi DIT Prof. Preksedis Ndomba na Mkuu wa Taasisi ya KIST Dkt. Mahmoud Abdulwahab Alawi, ambao walieleza dhamira yao ya kuhakikisha taasisi wanazoongoza zinatumia fursa hiyo kuboresha ubora wa elimu ya ufundi nchini.






# Fursa Vituo vya Umahiri >



# Vijana watakiwa kuchangamkia fursa za Vituo vya Umahiri kwa Maendeleo ya Taifa

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Hussein Omar, ametoa wito kwa vijana kote nchini kutumia kikamilifu fursa zinazotolewa na Vituo vya Umahiri ili kupata ujuzi utakaowawezesha kushiriki kikamilifu katika sekta muhimu za kiuchumi.

Dkt. Omar ametoa rai hiyo Agosti 07, 2025 jijini Dar es Salaam, katika kikao kilichowakutanisha wajumbe kutoka Jumuiya ya Vyuo Vikuu Afrika Mashariki, watekelezaji wa mradi, wawakilishi wa Benki ya Dunia, na viongozi mbalimbali wa Wizara.

Amesema kuwa elimu ya ufundi stadi na mafunzo yanayotolewa sasa yanalenga mahitaji halisi ya soko la ajira na kwamba msisitizo mkubwa umewekwa katika kuhakikisha wahitimu wanapata ujuzi wa vitendo unaowawezesha kuingia moja kwa moja katika ajira au kujiajiri.

Dkt. Omar alifafanua kuwa Vituo vya Umahiri vilivyoanzishwa kupitia Mradi wa EASTRIP vimejengwa kwa viwango vya kimataifa na vina vifaa vya kisasa vinavyowezesha utoaji wa mafunzo bora. Alitoa rai kwa vijana na wananchi kwa ujumla kuchangamkia fursa hizo ili kujiandaa kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya taifa.

Cosam Joseph, mmoja wa wajumbe kutoka Jumuiya ya Vyuo Vikuu Afrika Mashariki na ambao ndio wasimamizi wa Mradi Kikanda, alieleza kuridhishwa na utekelezaji wa mradi huo nchini Tanzania. Alisema majengo na vifaa vya kisasa vilivyowekwa vitawawezesha wanafunzi kupata ujuzi unaolingana na mahitaji ya soko la ajira ndani ya nchi, kikanda na kimataifa.



Usimamizi Rasilimali >

# Vijana watakiwa kusimamia kwa uwazi na uadilifu rasilimali za umma



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, ametoa wito kwa vijana wa Tanzania kuwajibika katika kusimamia matumizi sahihi ya rasilimali za umma, huku akisisitiza umuhimu wa kupambana na vitendo vya rushwa vinavyokwamisha maendeleo ya taifa.

Akizungumza tarehe 14 Agosti 2025 jijini Arusha, wakati wa ufunguzi wa Jukwaa la Uwajibikaji kwa Vijana 2025 lililoandaliwa na Youth Accountability Initiative Forum (YAIF), Prof. Mkenda alieleza kuwa vijana ni nguzo muhimu ya mabadiliko, na wanapaswa kuwa mstari wa mbele katika kuhimiza uwazi, uadilifu, na utawala bora.

"Uwajibikaji si jukumu la viongozi pekee, bali ni wajibu wa kila Mtanzania, hususan vijana ambao ndio nguvu kazi ya taifa," alisisitiza Prof. Mkenda.

Katika hotuba yake, Waziri Mkenda alii-pongeza YAIF kwa kuandaa jukwaa hilo lenye lengo la kuwahamasisha vijana kushiriki kikamilifu katika mijadala ya uwajibikaji. Alieleza kuwa hatua hiyo ni muhimu katika kujenga kizazi chenye maadili, uzalendo, na uelewa mpana wa masuala ya utawala bora.

Aidha, Prof. Mkenda aliwapongeza washiriki wa shindano la uandishi wa insha lililokuwa na maudhui ya "The Role of Public Accountability in the Proper Management of Public Resources", pamoja na Klabu Bora ya Mwaka 2024/2025 kwa mchango wao katika kusukuma mbele ajenda ya uwajibikaji miongoni mwa vijana.

Naye, Mkurugenzi wa Taasisi ya Wajibu, FCPA Ludovick Utouh, alisisitiza kuwa ushiriki wa vijana ni nguzo muhimu katika kuhakikisha rasilimali za umma zinasimamiwa kwa uadilifu na uwazi. Aliahidi kuwa taasisi yake itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuimarisha misingi ya uwajibikaji nchini.

Jukwaa hilo limehudhuriwa na vijana kutoka mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara, likiwa na lengo la kuendeleza mijadala ya uwajibikaji, uwazi, na uadilifu katika matumizi ya rasilimali za umma hatua muhimu kuelekea Tanzania yenye maendeleo jumuishi na endelevu.



Matumizi TEHAMA >



# Serikali kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Katibu Mkuu wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo amesema Serikali imeendelea kutekeleza kwa kasi mageuzi ya elimu nchini, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 sambamba na mwelekeo wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Prof. Nombo amebainisha hayo Agosti 18, 2025 Jijini Dodoma akizungumza na ujumbe wa Benki ya Dunia ulioongozwa na Meneja wa Programu za Elimu kwa Afrika Mashariki Bi. Muna Meky, ambapo amesisitiza kuwa, mageuzi hayo yanalenga kuimarisha maarifa, stadi stahiki na ujuzi kwa vijana sambamba na matumizi ya sayansi na teknolojia katika ufundishaji na ujifunzaji.



Amesema kuwa, mafanikio ya utekelezaji wa sera hiyo yanatokana na msaada wa kiufundi kutoka Benki ya Dunia na wadau mbalimbali wa maendeleo.

''Kwa msaada wa wadau wetu, tumeanza kujenga msingi imara wa namna ya kuimarisha ujuzi wa karne ya 21. Tunahitaji kuongeza matumizi ya TEHAMA katika kufundishia na kujifunzia ili kuendana na mahitaji ya sasa ya kidunia ya kidijitali'' amesema Prof. Nombo.

Aidha, Katibu Mkuu huyo ameeleza kuwa Serikali itahakikisha inatekeleza elimu ya lazima ya miaka 10, kuimarisha mafunzo ya walimu, pamoja na kuboresha elimu ya amali ili kuwajengea vijana maarifa, ujuzi na ubunifu unaohitajika katika soko la ajira la kitaifa, kikanda na kimataifa.

Meneja wa Programu za Elimu kwa Afrika Mashariki, Bi. Muna Meky, ameipongeza Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa utekelezaji mzuri wa miradi ya elimu inayofadhiliwa na Benki ya Dunia. Amesema kuwa Tanzania imeonyesha mafanikio makubwa katika utekelezaji wa programu za elimu katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Amesisitiza umuhimu wa kuendelea kuwekeza kwenye elimu ya msingi na kuhimiza matumizi ya mifumo jumuishi ya ufadhili kama vile Multi-Programmatic Approach (MPA), ambayo hutoa fursa ya kushirikisha rasilimali za kikanda na kimataifa, na kwamba Benki ya Dunia ipo tayari kushirikiana na Serikali katika kupanga vipaumbele vya ufadhili kwa miaka ijayo.

# Anuani za Taasisi zilizo chini ya Wizara

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU),**
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P 6562,
7 Mtaa wa Magogoni,
11479 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2113694, 2113691
Barua Pepe: es@tcu.go.tz

Mkurugenzi Mtendaji,
**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB),**
HESLB House, 1 Mtaa wa Kilimo -TAZARA,
Barabara ya Mandela,
P.O. Box 76068,
15471 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 736 665 533/ 739 665 533
Baruapepe: ed@heslb.go.tz

Katibu mtendaji,
**Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA),**
Eneo la Viwanda Mikocheni,
Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2624 au 32019,
14112 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2700493-6/9 na 22 2772423
Barua Pepe: esnecta@necta.go.tz

Mtendaji Mkuu,
**Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTVET),**
S.L.P 17007, DODOMA.
Simu: +255 26 2323 121 / 0733 77 77 51
Barua Pepe: info@nacte.go.tz

Mtendaji Mkuu,
**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM),**
Nunge Street, Old Catholic Church Road,
S.L.P 71, BAGAMOYO, PWANI.
Simu: +255 23 244 0216
Barua Pepe: adem@adem.ac.tz

Mkurugenzi Mkuu,
**Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH),**
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,
S.L.P. 4302,
14113 Kijitonyama,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 (022) 2771358/ 2774023/ 2700749
Baruapepe: dg@costech.or.tz

Mkurugenzi Mkuu,
**Taasisi ya Elimu Tanzania (TET),**
Plot 132, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P. 35094, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 0735 041168
Barua Pepe: director.general@tie.go.tz

Mkurugenzi Mkuu,
**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA),**
S.L.P 34578,
Mikocheni B, Bima Road,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Barua Pepe: info@tea.or.tz
dg@tea.or.tz

Mkurugenzi Mkuu
**VETA Makao Makuu,**
Plot No. 18, Central Business Park (CBP)
Barabara ya VETA,
S.L.P 802,
26 DODOMA.
Simu: +255 26 2963661
Baruapepe: info@veta.go.tz

Mtendaji Mkuu,
**Tume ya nguvu za Atomic Tanzania (TAEC)**
S.L.P 743,
23114 Engutoto, Block J, Plot No 216,
ARUSHA
Simu: +255 272 9700054
Barua Pepe:dg@taec.go.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM),**
Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani,
S.L.P. 35091, Mtaa wa Chuo Kikuu
16103 Dar es Salaam
Simu: +255222410700
Baruapepe: vc@udsm.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Ardhi University (ARU),**
Plot No. 3, Observation Hill Blok L,
University Road,
P.O. Box 35176, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 738 357 310-12
Baruapepe: aru@aru.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili (MUHAS),**
9 Barabara ya Umoja wa Mataifa,
Upanga Magharibi,
S.L.P. 65001,
11103 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2150302-6
Baruapepe: vc@muhas.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA),**
S.L.P 3000,
Barabara ya Edward Moringe, Mtaa wa Kilimo,
01 MOROGORO
Simu: +255 23 260511-4
Barua Pepe: sua@sua.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Mzumbe (MU),**
S.L.P 1, MOROGORO
Simu:
Barua Pepe: mu@mzumbe.ac.tz
info@mzumbe.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),**
S.L.P 259,
Mtaa wa Benjamin Mkapa,
Jengo la Benjamin Mkapa,
41107 DODOMA.
Simu: +255 26 2310001/2/3
Barua Pepe: vc@udom.ac.tz
relations@udom.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT),**
S.L.P. 23409,
14110 Open University Road,
Kinondoni Municipality,
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2668820/ 2668992
Baruapepe: vc@out.ac.tz

RASI wa Chuo,
**Chuo Kikuu kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE),**
Taifa Road Next to Benjamin Willium,
S.L.P 2329,
15105 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2850975
Barua Pepe: principal@duce.ac.tz
dpacademic@duce.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ushirika Moshi,**
06 Barabara ya Sokoine Moshi,
S.L.P 474
KILIMANJARO
Simu: +255 272 751 833
Barua Pepe: info@mocu.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kushiriki Cha Elimu Mkwawa (MUCE),**
Mtaa wa Mkwawa Chuo,
S.L.P. 2513,
51111 IRINGA CBD.
Simu: +255 26 2702 751
Baruapepe: principal@muce.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST),**
S.L.P. 131,
Barabara ya 01 MUST,
01 MBEYA.
Simu: +255(0)25 2957542/4
Barua pepe: vc@mustnet.

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NMIST),**
Kampasi ya Tengeru, Barabara ya Nelson Mandela,
S.L.P. 447,
23301 TENGERU, ARUSHA
Simu +255 272970001
Baruapepe: vc@nm-aist.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere,**
S.L.P 976, Butiama, MARA
Simu:
Barua Pepe: info@mjnuat.ac.tz

Mkurugenzi
**Bodi ya Huduma za Maktaba (TLSB),**
27 Mtaa wa Bibi Titi Mohamed,
S.L.P 9283
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2150048/9
Barua Pepe: info@tlsb.go.tz

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Taifa ya UNESCO,**
7 Magogoni Street,
P. O. Box 20384,
11479 DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2126598/ 22 2134292
Baruapepe: info@natcom.go.tz

Mkurugenzi,
**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)**
23 Mtaa wa Bibi Titi Mohammed,
S.L.P. 20679,
11103 DAR ES SALAAM
Simu:
Baruapepe: info@iae.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ufundi Arusha (ATC),**
Junction of Moshi-Arusha and Nairobi Roads,
P.O. Box 296,
23105 ARUSHA.
Simu: +255 (0) 27-297 0056
Baruapepe: rector@atc.ac.tz/pro@atc.ac.tz

Mkurugenzi,
**Kituo cha Maendeleo Dakawa,**
S.L.P 1733,
MOROGORO.

Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT),**
Kona ya Bibi Titi na Barabara ya Morogoro
S.L.P 2958
11104 DAR ES SALAAM
Simu:
Barua Pepe: principal@dit.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA),**
30 Barabara ya Kibada,
S.L.P 9193,
17107 Kigamboni,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Baruapepe: rector@mnma.ac.tz